# Itikadi za Ujinsia katika Maumbo ya Majina ya Kikuria

*Roseline Kasuma[1], James Ogola[2] na Sangai Mohochi[3]*
[1]*Chuo Kikuu cha Rongo*
[2]*Chuo Kikuu cha Laikipia*
[3]*Chuo Kikuu cha Kibabii*

**Ikisiri**

**Majina ni vipengele vya lugha ambavyo hutaja mtu, kitu, hali, mahali, dhana na tendo na huweza kufunua itikadi na matukio katika maisha ya wanajamii. Itikadi ni mawazo ambayo humwongoza kila mtu ulimwenguni katika kutenda anayotenda na hivyo kuhalalisha au kuharamisha matendo anayoyafanya. Makala haya yanajikita katika kuchanganua jinsi maumbo ya majina ya Kikuria katika jamii ya Wakuria iliyoko nchini Kenya hushamirisha itikadi za ujinsia. Itikadi za ujinsia ni imani, mielekeo na mitazamo inayoongoza jamii kuhusu mgawanyo wa majukumu kwa kuangalia jinsia. Lengo kuu la makala haya ni kuainisha jinsi maumbo ya majina ya Kikuria hudumisha na kuendeleza itikadi za ujinsia. Data iliyotumika katika makala haya ilikusanywa kwa njia ya mahojiano ya ana kwa ana na majadiliano ya makundi. Ukusanyaji na uchanganuzi wa data uliongozwa na Nadharia ya Onomastiki. Nadharia hii imekuwa dira katika kubainisha maumbo ya majina ya Wakuria na jinsi maumbo haya huakisi itikadi za ujinsia katika jamii ya Wakuria. Utafiti wetu uliweza kubainisha kuwa vipo vipashio ambavyo hudokeza jinsia na shughuli inayohusishwa nazo au nafasi yake katika jamii. Kwa misingi hii, utafiti wetu ulibainisha kuwa jinsia ya kiume kwa mujibu wa majina yao yaliyoteuliwa kiitikadi, ilitengewa shughuli na nafasi zilizoikweza ikilinganishwa na jinsia ya kike.**

**Maneno Muhimu:** *Itikadi za Ujinsia, Maumbo, Majina, Shughuli, Wakuria*

## Utangulizi

Suala la ujinsia limekuwa kitovu cha tafiti nyingi katika jamii mbalimbali.Tafiti hizi katika jamii anuwai zimebainisha uhusiano wa kijinsia miongoni mwa wanajamii. Katika baadhi ya kazi hizi mwanamume amesawiriwa kama kiumbe aliyekwezwa katika jamii na mwenye kuhodhi nyenzo zote za kiuchumi. Kwa upande mwingine, mwanamke amejitokeza kama kiumbe ambaye mahali pake ni jikoni na mlezi wa watoto wa mumewe. Aidha, amesawiriwa kama mgeni katika maskani yao, kwani ataoleka na kuambaa makao yake ya awali. Mitazamo hii inashadidiwa na itikadi za jamii husika. Miongoni mwa mambo yanayodhihirisha mitazamo hii katika jamii mbalimbali ni majina wanayopewa wanajamii. Hili linamaanisha kuwa itikadi ni sehemu muhimu inayochangia katika kuelewa jamii kikamilifu.

Majina ya wanajamii huweza kuelekeza jinsi wanajamii huuona ulimwengu wao kitamaduni, kiitikadi na matukio ya kihistoria katika maisha yao. Kama anavyosema Bertills (2003), katika lugha na tamaduni nyingi, jina pekee huchukuliwa kuwa kipashio muhimu cha kurejelea mtu. Kufuatia hili inatokea kuwa uchanganuzi wa maumbo ya majina huweza kuibua itikadi za kijinsia zinazoshamirishwa katika lugha husika. Hata hivyo, tafiti kuhusu jinsi itikadi za jamii zinavyojitokeza na kuendelezwa kupitia kwa maumbo ya majina ya watu si dhahiri. Ni kutokana na pengo hili ambapo utafiti umechanganua itikadi za ujinsia katika maumbo ya majina katika jamii ya Wakuria nchini Kenya.

Utafiti uliofanyika ulikuwa wa kiuthamano na ulifanyika katika kaunti ya Migori nchini Kenya mwaka 2020, walengwa wakiwa ni Wakuria. Sampuli iliyotumika iliteuliwa kimaksudi na kimapokezano. Data ilikusanywa kwa kutumia mahojiano na majadiliano ya makundi. Jumla ya watafitiwa 42 walihojiwa ana kwa ana 24 wakiwa wa jinsia ya kiume na 18 wa jinsia ya kike. Aidha, majadiliano ya makundi yalifanyika manne, mawili kwa kila jinsia. Kila kundi lilikuwa na watu

wanane. Mwongozo wa usaili ulitumika katika kukusanya data. Katika uchanganuzi, ni majina ya asili yaliyosheheni itikadi za ujinsia yalizingatiwa.

**Maumbo ya Majina**

Jamii nyingi huthamini majina na shughuli ya ujinaishaji. Hii ni kwa sababu majina hueleza utamaduni wao, falsafa, mawazo, mazingira, imani na lugha yao. Kama anavyoeleza Zanawi (1993), jina huumba mtu kwa maana jina analopewa mtu hujenga mtazamo kwa wale wanalolisikia kabla hawajamfikia mrejelewa.

Katika muktadha wa ujinaishaji, ujinsia huzingatiwa kwanza, kisha hali ya kijamii na kiuchumi ya wazazi na wakati wa kuzaliwa. Kwa vile majina yana maana kijamii, mtu hutarajiwa kuishi kulingana na maana yake au kulifanyia marekebisho chanya (Agyekum, 2006). Kinachotokea ni kuwa watu hutarajia nguvu iliyo katika maneno yanayounda jina kuakisi maisha ya warejelewa kwa njia iliyo hasi au chanya. Kwa maana hiyo jina la mwanajamii huwa ni suala muhimu katika jamii nzima. Majina hutarajiwa kufinyanga malezi ya watoto, mienendo na ujamiishaji wao na ni dhahiri kuwa msingi wa ufinyanzi huu huwa kwenye maumbo ya majina yenyewe.

Majina kama maneno yanayopatikana katika lugha husika hupaswa kuwa na ruwaza ya maumbo na muundo unaoyaunda (Marjie- Okyere, 2015). Uchanganuzi wa maumbo ya majina umeshughulikiwa na watafiti wengi na kama anavyosema Malande (2011) majina huweza kuainishwa kwa misingi ya maumbo yake. Aidha, umbo la jina hutoa msingi wa maelezo ya maana yake (Ntahombaye katika Batoma (2009). Mathalan, Mutegi (2017) alibainisha mifumo ya ujinaishaji ya Wameru, kupambanua semantiki ya majina na kutathmini mielekeo ya watu kuhusu majina yao. Vile vile, Gitau (2012) alichanganua kisemantiki nomino za Kigikuyu. Katika utafiti wake alichunguza jinsi nomino za Kigikuyu huweza kuchanganuliwa kisemantiki. Ilidhihirika kuwa vipashio vya kifonolojia huwa tofauti kimaana.

Jina la Kikuria lina sehemu tatu: kiambishi awali, kiambishi cha ngeli na mzizi (Mwita, 2012). Majina yote huwa na kiambishi awali isipokuwa vitenzi-jina ambavyo huwa na mofu kapa. Nomino hizo huwa na wingi na umoja. Mwita (keshatajwa) alishughulikia majina au nomino kwa jumla na lengo lake kubwa lilikuwa kubainisha muundo wa majina ya Wakuria. Makala hii inatofautiana na kazi zilizojadiliwa hapo juu kwa vile inalenga kuchanganua maumbo ya majina ya Wakuria yenye kuhodhi itikadi za ujinsia.

Ni muhimu kutaja kuwa majina ya wanajamii yana maana ya nje na ya ndani, kwamba majina huhusiana na sehemu nyingine za utamaduni na huashiria umoja na utambulisho wa jamii hiyo (Gudeta, 2014). Wakishadidia dhana hii, Jauro na Wappa (2013) walibainisha kuwa maana ya majina katika ruwaza za ujinaishaji wao huweza kukisiwa kutokana na vipengele vya maumbo yao suala linalochanganuliwa katika makala hii. Majina pia huelekeza katika kutambua ujinsia. Ruth (1992) anaeleza kuwa hii huwezekana kwa kuchanganua vipashio vinavyounda majina hayo na jinsi vipashio hivyo hujenga na kuendeleza itikadi za ujinsia katika jamii ya Wakuria.

Okal (2018) akielelezea majina anasema kuwa majina yenye kueleza jinsia ya kiume au kike yana mzizi sawa. Tofauti hujitokeza kwenye mofimu zinazoambishwa kabla au baada ya mzizi husika. Anaendelea kusema kuwa zipo mofimu katika jamii nyingi nchini Kenya ambazo zinapotumika katika jina basi huweza kueleweka moja kwa moja kuwa mrejelewa ni wa kiume au kike. Mfano, katika jamii ya Wajaluo {O-} hurejelea jinsia ya kiume huku {A-} ikirejelea jinsia ya kike. Mifano mingine ni kama:

| **Jamii** | **Kiume** | **Kike** | **Maana** |
|---|---|---|---|
| Wajaluo | **O**doyo | **A**doyo | Msimu wa kupalilia. |
| Waluhya | **Wa**njala | **Na**njala | Msimu wa njaa. |
| Wakalenjin | **Kip**talam | **Chep**talam | Msimu wa nzige. |
| Wakamba | Mwend**wa** | Mwend**e** | Anayependwa. |

Ingraham katika Barry na Harper (2013) vilevile alionyesha kuwa katika Utawala wa Waroma, majina yaliyotolewa kwa jinsia ya kike na kiume yalikuwa sawa isipokuwa tamati ilikuwa na {-a} kuashiria jinsia ya kike na {-us} kuashiria jinsia ya kiume. Mathalan, Claudi**a** na Claudi**us**.

Okal na Ingraham (washatajwa) hawakupiga hatua zaidi ya kubainisha majina kijinsia katika kazi zao suala ambalo makala hii inashughulikia kuonyesha itikadi zinazoendeleza ujinsia katika maumbo ya majina haya hususan jamii ya Wakuria.

**Uchanganuzi wa Maumbo ya Majina ya Kikuria**

Majina ya Kikuria yana mizizi ya vitenzi, vivumishi na nomino. Ni katika mizizi hii ambapo mofimu huambikwa ili kuunda jina. Mofimu hizi huambikwa kwa jinsi ambayo hubainisha jinsia ya mrejelewa. Lugha ya Kikuria kama lugha nyingine za kibantu ni lugha ambatishi. Uambatishaji ni mbinu ya kimofolojia ambapo maneno tata huundwa kwa kuunganisha mofimu bila kubadilisha fonimu zake. Katika lugha ambatishi, mofimu huunganishwa kwa njia ambayo ni rahisi kutambua mipaka yake. Aidha, kila mofimu hubeba maana moja. Mofimu ni kipashio kidogo kabisa katika umbo la neno kilicho amilifu na ambacho hakiwezi kuvunjwa au kugawanywa katika vipande vingine vidogo bila kupoteza uamilifu wake (Mgullu, 1999).

Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa, aina mbili za majina zilipatikana: majina yenye asili ya Kikuria na majina yenye asili ya kigeni ambayo yalikuwa yamesilimishwa ili kuoana na lugha ya Kikuria. Ni kawaida kwa lugha kuwa na majina ya asili na mengine ya kigeni, na kwamba yale ya kigeni hupewa nafasi kwa kusilimishwa (Muzale, 1998). Makala hii inajikita katika maumbo ya majina ya asili katika jamii ya Wakuria na itikadi za ujinsia zinazoshamirishwa.

Ni muhimu kutaja kuwa kazi hii imeongozwa na Nadharia ya Onomastiki Mkabala wa Onomastiki wa Raper (1987). Katika mtazamo huu Raper (keshatajwa) anasema kuwa Onomastiki ni sayansi au uchunguzi wa asili na maumbo ya majina. Kwa mujibu wa Raper, Onomastiki hujikita katika majina ya pekee ya watu. Jina la pekee kama ishara nyingine ile ya kiisimu huhusisha mfululizo wa sauti ambazo huwasilishwa kwa grafu na ina 'fahiwati' au 'maana.' Aidha, ishara hii ina jukumu la kurejelea au kuwakilisha viziada vya kiisimu. Isitoshe, uchunguzi wa kionomastiki hujikita katika dhana kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya lugha ya watu na shughuli zao za kitamaduni. Ni kwa misingi hii ambapo utafiti huu ulichunguza maumbo ya majina ya Kikuria kwa kujikita kwenye ukweli kuwa majina hayo yanahusiana na shughuli mbalimbali za utamaduni wa jamii kama ifuatavyo:

***Majina yanayotokana na mzizi wa kitenzi***

i) **Chacha**

cha-cha ≥ wa – me-kuja

***ch-*** – mofimu ya wingi kuashiria kuwa ng'ombe wamekuja.

***ch-*** – mzizi.

***a*** – kiishio.

***{cha-}*** ni mofimu inayowakilisha dhana ya wingi katika jina *Chacha*. Kinachorejelewa katika wingi huu ni ng'ombe ambao ni sehemu ya maisha ya mwanamume katika jamii ya Wakuria. Shughuli ya msingi ya Wakuria ilikuwa ufugaji ambapo mifugo hasa ng'ombe walipatikana mara nyingi kwa njia ya "kuchukua" kutoka kwa majirani wao Wamasai. Wakuria waliamini kuwa ng'ombe ni wao waliopewa na mzazi wao wa kwanza – *Monto*. Kwa hivyo, walipoona jamii nyingine ikiwa na mifugo hawa vijana walienda kuwachukua na wala si kuiba kama ilivyochukuliwa. Kwa maana hiyo, mtoto alipopewa jina hili kama mtoto wa kiume ilimpa ushujaa kwamba alizaliwa wakati wa ushindi wa kurejesha mali yao nyumbani na kwamba alitakiwa kukua na kujiunga na wanaume wengine washindi katika shughuli hiyo. *Chacha* ni jina la ushindi. Mofimu {cha-} kwa hivyo hushamirisha itikadi kuwa mtoto wa jinsia ya kiume anayepewa jina *Chacha* hutakiwa kujitahidi muda wote kuhakikisha kuwa hapungukiwi kama alivyo mshindi. Mtazamo wa Wakuria kuhusu jina hili unashabihiana na Obeng (2001) katika Mphela (2010) kuwa majina katika utamaduni wa Kiafrika ni vielelezi vya imani, ndoto na matamanio ya watumiaji wake.

**ii) Mwita**

Mwita- Mw- ita > ua

***Mw*** – mofimu hii huwakilisha nafsi katika umoja.

***it-*** – mzizi.

***a*** – kiishio.

Jina *Mwita* lina maana ya mwuaji. Utafiti uliofanyika ulibaini kuwa, Wakuria hawakuendekeza suala la kutoa mtu uhai lakini ilipotokea katika vita mtu huyo alionekana shujaa na mtoto wa jinsia ya kiume alipozaliwa katika familia hiyo alipewa jina Mwita kuwa yeye ni shujaa aliye na uwezo wa kumwangamiza adui. Mtoto wa jinsia ya kike alipozaliwa hakupewa jina hili. Dhana ya ushujaa katika jamii ya Wakuria kwa mujibu wa utafiti uliofanyika lilihusishwa na jinsia ya kiume tu.

**iii) Boke**

*Boke – bookeye > kumekucha.*

***Bo***-ke

***Bo*** – mofimu ya wakati/hali.

***-k-*** - mzizi.

***e –*** kiishio.

Jina hili hutumika kiistiari. *Boke* lina maana ya kucha na hutolewa kwa mtoto wa jinsia ya kike. Kucha ni ishara ya kuja kwa utajiri katika jamii, mwanzo mpya. Jinsia ya kike huonekana kama kivutia mali. Mali katika jamii ya Wakuria hunasibishwa na wingi wa ng'ombe. Mnata (2012) anaeleza kuwa familia ambayo haina mtoto wa kike kwao huwa kama usiku wa kiza ndiposa anapozaliwa mtoto wa kike husemekana kumepambazuka kwani atakapoolewa ng'ombe ambao ndio mahari watamiminika nyumbani kwao.

***iv) Mogesi***

*Mogesi* - *-gesa* > *vuna*

*Mo-gesa(i)* – m- vuna(i) – anayevuna.

*Mo* - mofimu ya nafsi ya kike, umoja.

*ges-* - mzizi.

*i* – kiishio.

Jina *Mogesi* hutokana na kitenzi *-gesa* chenye maana ya –vuna. *{mo-}* ni mofimu inayowakilisha mtendaji wa jinsia ya kike. Uvunaji katika jamii ya Wakuria ni shughuli iliyotengewa jinsia ya kike. Mtoto wa kike anapozaliwa wakati wa uvunaji hupewa jina Mogesi na hujamiishwa kujihusisha kikamilifu katika shughuli hii. Itikadi ya ujinsia inayoshamirishwa na jina hili ni kwamba jinsia ya kike ni jinsia inayotakiwa kujihusisha na shughuli za shambani hususan kuvuna.

**v) Magesa/Magesi**

*Magesa (i) – ma-ges-a* > *mavuno*

*Ma* – Mofimu inayowakilisha wingi.

*ges-* – mzizi.

*a* – kiishio.

Jina hili huundwa kutokana na kitenzi *-gesa* - vuna. *{ma-}* ya wingi huleta dhana ya jinsia ya kiume japo wanaovuna ni jinsia ya kike. Mofimu hii huwa kumbukumbu kwa mrejelewa kama jinsia ya kiume kuwa hatakiwi kupungukiwa hasa kama mkuu wa familia yake. Pili, yeye ndiye mmiliki wa wanaovuna ambao ni jinsia ya kike. Utafiti uliofanyika ulibainisha kuwa suala hili huwafanya wanaume wengi kuoa wanawake wengi kwa lengo la kuwa na wafanyakazi wengi shambani ili mavuno yawe mengi.

**vi) Murimi**

*Murimi* > *mu-rim-i* > *m –kulim-a*

*Rima* - lima

*Mu* – Mofimu inayowakilisha nafsi ya jinsia ya kiume katika umoja.

*rim-* – mzizi.

*i-* Kiishio.

*Murimi* ni mtu ambaye ana ujuzi na uzoefu wa kilimo. Jina hili hupewa jinsia ya kiume. Jina *Murimi* limeundwa kutokana na kitenzi *-rema* – lima. *{Mu-}* huwakilisha jinsia ya kiume katika umoja. Kwa mujibu wa utafiti wetu *Murimi* ni mtu mwenye bidii ya kuamka mapema na kwenda shambani kutegemea msimu kulima, kupanda, kupalilia au kuvuna. Bidii hii huhitajika kuwa nayo mtoto wa jinsia ya kiume ili kuhakikisha familia yake ina chakula cha kutosha. Ni muhimu kutaja kuwa shughuli ya kulima huwa ya jinsia ya kike na wajibu wa mwanamume huwa ni kusimamia. Hivyo, mavuno yalipojibu sifa zilimwendea mume kuwa yeye ni *Murimi*. Mofimu {Mu-} hushamirisha sifa hizi.

**vii) Nyakorema**

**Nya – ko –rem –a > wa – ku – lim -a**

Jina hili ni kinyume cha *Murimi* na hupewa mtoto wa jinsia ya kike. {Nya-} hushamirisha dhana ya umilikaji. Jina hili hupewa mtoto wa kike ambaye huzaliwa ama mama yake akilima au msimu wa kulima. Jina hili huendeleza dhana kuwa jinsia ya kike ni ya kufanya kazi ya kulima na mtoto wa kike hujamiishwa kujiimarisha katika shughuli hii.

**viii) Gati**

*Gat-i-a > a – gat – i – a > a – ka –pasu - a*

Jina Gati lilitokana na kitenzi *agatia-* akapasua. Asili ya jina hili ni maumbile ya mwanamke ambayo hufungamanishwa na shughuli zake za kila siku. Kilonzo (2015) anashadidia kuwa utamaduni wa Kiafrika unaipa jinsia ya kike utambulisho wa mtumishi wa nyumbani, huku wanaume wakitambulishwa na utamaduni huu kama watu wasiojihusisha na shughuli za nyumbani kwa kiasi kikubwa. Mtoto wa jinsia ya kike alipewa jina hili alipozaliwa wakati wanawake wanapasua kuni. Kuni hizi hupasuliwa kwa minajili ya maandalizi ya *(inyangi)* sherehe mbalimbali mathalani tohara na arusi. Kutokana na jina hili, shughuli ya kupasua kuni kwa ajili ya matumizi ya sherehe au jikoni hunasibishwa na jinsia ya kike. Umbo la jina hili hujamiisha warejelewa kuhusu jinsi ya kutafuta kuni kwa ajili ya mapishi miongoni mwa kazi nyingine.

Mtazamo mwingine kuhusu asili ya jina hili ni kutokana na kitenzi *goteka-* kupasuka. Suala la mwanamke kushika mimba lilimstaajabisha sana mwanamume wa Kikuria. Akaona kana kwamba mwanamke amekuwa na nguvu ambayo yeye hana ikizingatiwa kuwa mwanamke alichukuliwa kuwa kiumbe dhaifu na jamii. Mimba hii iliwapa maswali kuwa ni nini kiko ndani na kitatokaje! Mwanamke huyu alipojifungua ikaonekana alipasuka katikati ya miguu ili mtoto atoke. Kwamba maumbile ya sehemu yake ya uzazi pia yalichangia kusaidia kupasuka yakilinganishwa na ya mwanamume. Kutokana na maajabu haya kwamba mwanamke alipojifungua mara ya kwanza alipasuka mtoto akapewa jina *Gati* kwamba alimpasua mama yake. Ni dhahiri kuwa umbo la jina hili huendeleza dhana kuwa kazi ya jinsia ya kike ni kujifungua ili kuendeleza kizazi.

**ix) Meng'anyi**

*Me – ng'any - i > M – ham – a – ji.*

Jina hili hupewa mtoto wa jinsia ya kiume. Jina hili huundwa kutokana na kitenzi *ng'anya* – hama. Wakati wa majanga au vita, Wakuria walilazimika kutorokea kulikokuwa salama. Wakati wa tukio hili watu walijawa na wasiwasi na hofu nyingi. Wanaume walisemekana kuwa walikuwa wakihamia kulikokuwa salama. Wao si waoga ndio maana hawakutoroka bali walihama. Mtoto wa jinsia ya kiume aliyezaliwa wakati huu alipewa jina Meng'anyi (mhamaji) kuendeleza dhana kuwa hatari inapotokea jinsia ya kiume huhama. Jina hili hushadidia itikadi kuwa jinsia ya kiume ni mashujaa na janga linapotokea wao hupaswa kuhama tu bali si kuogopa.

**x) Mong'osi**

*Mo – ng'os – i > M – torok – a – ji*

Jina Mong'osi limetokana na kitenzi ng'osa – toroka. *{Mo-}* huwakilisha nafsi ya jinsia ya kike katika umoja. Asili ya jina hili ni kuwa wakati jamii ya Wakuria walipopata majanga au vita kutokea walilazimika kutoka katika eneo waliloishi na kuenda kulikokuwa salama**.** Wanawake walitangulia na

watoto kisha wanaume walifuata wakiwa na mifugo yao. Katika kufanya hivi, jamii ya Wakuria walichukulia kile kitendo cha kuondoka kwa wanawake kuwa kilitokana na woga ndiposa walitoroka ikilinganishwa na wanaume ambao walihama. Kutokana na dhana hii, mtoto wa jinsia ya kike ambaye huzaliwa wakati wa kuhama huitwa Mong'osi na hujamiishwa kuamini kuwa yeye ni mwoga na wakati wa hatari anapaswa kutoroka huku wale wa kiume wakihama.

**Majina Yanayotokana na Mizizi ya Nomino**

**i)** ***Machera*** *– ma- chera > enchera*

*Ma-chera* – ma-jia

*Ma-* mofimu ya wingi.

-*cher* - – mzizi.

*a-* kiishio.

*Machera* lina maana ya majia mengi. *{ma-}* inaendeleza dhana ya wingi na ukuu ulio kwenye ukubwa wa njia sifa anazotakiwa kuwa nazo mtoto wa jinsia ya kiume katika jamii ya Wakuria. Jina hili hupewa mtoto ambaye huzaliwa njiani.

**ii) Nyagoncher**a

Nya – go – ncher – a > wa – nji - a – ni

Nya – mofimu inayowakilisha jinsia ya kike.

*Nyagonchera* lina maana ya mtu wa njiani. *{Nya-}* inabainisha kuwa kazi ya *Nyagonchera* ni kupitapita njiani ikizingatiwa kuwa mwanamke katika jamii ya Wakuria hutarajiwa kuwa mtu aliyetulia nyumbani ili kutekeleza majukumu yake ya ndani kikamilifu. Jina hili hupewa mtoto wa jinsia ya kike anayezaliwa njiani.

**iii) Matiko**

*Matiko – ubutiko* > usiku.

*Ma – tiko*

*Ma* - mofimu ya wingi.

-*tik*- – mzizi.

-o – kiishio.

Jina *Matiko* linaendeleza dhana ya ukubwa na wingi wa usiku. Kimsingi, usiku ni wenye giza na giza huogofya. *{ma}* inamjengea mrejelewa sifa za ushujaa uliomkubwa na mwingi kiasi cha kutotetereshwa na giza usiku.

**iv) Wankio**

*Wa – inkio > Wa - asubuhi*

*Wa – mofimu ya a – unganifu.* Mofimu hii huwakilisha umilikishi katika jamii ya Wakuria.

-*inkio – asubuhi (nomino).*

Kwa mujibu wa utafiti, mtoto wa jinsia ya kike anapozaliwa muda wa asubuhi pamoja na yule anayezaliwa usiku huitwa *Wankio* (wa asubuhi). Jina hili huashiria kuwa jinsia ya kike ni yenye uoga na hupaswa kutembea tu kunapopambazuka. Kwa upande mwingine, kupambazuka huwa taashira kuwa kuzaliwa kwa mtoto wa kike huleta matumaini kuwa familia itapata mali (ng'ombe) mahari pindi atakapoolekа.

**v) Wambura**

*Wambura – imbura – mvua*

*Wa - imbura > wa- mvua*

*Wa-* mofimu ya a- unganifu inayowakilisha nafsi ya kiume.

-*mbura* – mzizi.

Mtoto wa jinsia ya kiume anapozaliwa msimu wa masika (mvua) hupewa jina *Wambura*. Jina *Wambura* linatokana na jina *imbura* lenye maana ya mvua. Mvua huhusishwa na neema kwani chakula na maji huwa ya kutosha kwa binadamu na mifugo wake. Kwa vile jukumu la kutosheleza mahitaji ya jamii huwa la mwanamume, jina hili kupitia kwa mofimu *{wa-}* hushamirisha itikadi kuwa mwanamume huwa ameneemeka kiasi cha kuauni familia yake.

**vi) Wanchara**

*Wa – nchara > wa njaa.*

*Wa*- mofimu ya a- unganifu kuwakilisha nafsi ya kike umoja.

*-nchara* – mzizi wa nomino inchara (njaa).

Mtoto wa jinsia ya kike anayezaliwa wakati wa njaa huitwa *Wanchara*. Kwamba yeye ni wa njaa. Sifa ya ukosefu hainasibishwi na jinsia ya kiume katu kwani jamii huiona kama udhaifu ambao huhusishwa tu na jinsia ya kike.

**vii) Nyanswi**

*Nyanswi – inswi > samaki*

*Nya-nswi > wa-samaki*

*Nya – mofimu ya a-unganifu inayowakilisha nafsi ya kike, umoja.*

*-nswi – mzizi wa nomino inswi.*

Mtoto wa kike anayezaliwa wakati mwanafamilia yuko kwenye uvuvi hupewa jina *Nyanswi*. Utafiti uliofanyika ulibaini kuwa {*Nya-}* haikuleta dhana ya umiliki tu bali usafi. Kwamba mtoto wa kike anatakiwa kuwa ameoga safi sawa na samaki majini. {nya-} katika jina hili, huendeleza itikadi kuwa jinsia ya kike hutakiwa kuwa safi.

**viii) Maswi**

*Maswi – ma- swi > samaki wengi wakubwa.*

*Ma - mofimu inayowakilisha ukubwa katika wingi.*

*-swi- mzizi wa nomino inswi*.

Neno *maswi* linatokana na *ichinswi*. *Ichinswi* ni samaki. *Maswi* ni ukubwa wa *ichinswi*. {*Ma*-} huleta dhana ya ukubwa katika hali ya wingi. Mtoto wa jinsia ya kiume anayezaliwa wakati babake mzazi akiwa ameenda kuvua samaki hupewa jina hili. {ma-} katika jina hili hushamirisha itikadi kuwa jinsia ya kiume huhusishwa na ukubwa. Kutokana na majina haya- *Nyanswi na Maswi*, usafi kwa jinsia ya kike ulikuzwa kinyume na jinsia ya kiume.

***ix) Nyangwe***

*Nyangwe –ingwe > chui.*

*Nya-ngwe* – wa chui.

*Nya*- mofimu ya a- unganifu inayowakilisha nafsi ya kiume, umoja.

*-ngwe* – mzizi wa nomino ingwe.

Jina Nyangwe hupewa mtoto wa kiume ili kumrithisha sifa za mnyama huyu. *Engwe* (chui) ni myama mkali na hodari miongoni mwa wanyama mwitu. *{Nya-}* katika jina hili, humjamiisha mtoto wa jinsia ya kiume kuamini kuwa yeye ni mkali na hodari sawa na chui hasa wakati wa hatari anapohitajika kujitetea au kutetea jamii yake.

***xi) Nyankwi***

*Nya – nkwi >* wa kuni.

*Nya* – mofimu ya a-unganifu inayowakilisha jinsia ya kike, umoja.

*-nkwi* – mzizi wa nomino ichinkwi (kuni).

Jina hili hupewa mtoto wa kike ambaye huzaliwa huku mama yake akiwa katika harakati za kutafuta kuni. *{Nya-}* huleta dhana kuwa mtoto huyu ni wa kuni, kwamba shughuli yake ni kutafuta kuni na hujamiishwa kuwa hivyo.

**Mizizi ya Vivumishi**

Baadhi ya majina katika jamii ya Wakuria hutokana na vivumishi. Kivumishi ni neno ambalo hutoa maelezo zaidi kuhusu nomino (Riro, 2012). Majina haya ni kama yafuatayo.

**i) Babere**

*Babere – ba-bere >wa wili.*

*Ba- Mofimu inayowakilisha wingi.*

*-bere – mzizi wa kivumishi cha idadi babere (wawili).*

Jina hili hupewa mtoto wa jinsia ya kiume pale ambapo pacha wa jinsia tofauti walizaliwa. Jina hili ni utambulisho wa watoto pacha. Yule mtoto wa pili ambaye ni wa jinsia ya kike hupewa jina tofauti kwa kuzingatia ruwaza iliyopo. Mofimu *{ba}* huwakilisha wingi na katika muktadha huu mofimu hii hudhihirisha jinsi mtoto wa jinsia ya kiume ni muhimu katika jamii ya Wakuria akilinganishwa na wa kike.

**ii) Kimwamu**

*Kimwamu – imwamu > eusi*

*Ki- mofimu inayowakilisha umoja.*

-mwamu – mzizi wa kivumishi cha sifa.

*Kimwamu* kwa misimu ya kisasa huoana na mwezi wa nne. Huu ni msimu ambapo Wakuria huanza kupalilia. Msimu huu pia huwa na mvua nyingi. Neno *kimwamu* hutokana na weusi wa mawingu ya mvua. Kwa hivyo, *Kimwamu* ni kitu cheusi. Weusi huu pia husemekana kuwa ni ule unaotokana na kijani kibichi kinachochipuka baada ya mvua nzito. Kijani kibichi ambacho kwa wafugaji huwa ni lishe tosha kwa mifugo wao. Hii ndio husababisha mtoto wa kiume anayezaliwa wakati huu kupewa jina *Kimwamu. {Ki-}* ni mofimu inayowakilisha dhana ya umoja wa kitu kisichobainika.

**iii) Nyairabu**

*Nyairabu – irabu > eupe.*

*Nya – irabu.*

*Nya - mofimu ya umoja inayowakilisha nafsi ya kike.*

*-irabu* – mzizi wa kivumishi cha sifa.

Jina *Nyairabu* hutokana na jina Kerabu. *Kerabu* - kitu cheupe, ni msimu wa kupumzika na huja baada ya *Kimwamu.* Weupe huu hutokana na dhana kuwa kazi nzito za shamba huwa zimeisha, kwa hivyo ni kana kwamba huwa kumepambazuka. Watu hukaa tu nyumbani isipokuwa wanaume ambao huenda kulisha ng'ombe. Mtoto wa kike anapozaliwa wakati huu hupewa jina *Nyairabu* si kwamba ni mweupe bali kwa sababu amezaliwa msimu ambao huwa hakuna kazi. Kwa mujibu wa itikadi za jamii ya Wakuria kukaa bila kazi ni dalili ya uzembe sifa inayohusishwa na jinsia ya kike. Hii inashadidia usemi wake Blum katika Olatunji na wenzake (2015) kuwa majina ya misimu hutawala maisha ya mtoto kwa kiwango fulani.

**Mjadala Kuhusu Maumbo ya Majina ya Wakuria**

Makala haya yamejadili itikadi za ujinsia katika maumbo ya majina asili katika jamii ya Wakuria nchini Kenya. Makala haya yamebaini kuwa maumbo ya majina haya hugawa jinsia kwa mujibu wa majukumu yake kulingana na matarajio ya jamii. Ni dhahiri kuwa mofimu {mo-} inapotumika katika jina lililotengewa jinsia ya kiume huleta dhana chanya. Mathalani, *Mogendi*, jina linaloashiria mtu aliye na uwezo wa kutembea masafa marefu bila kuchoka. Hili huendeleza itikadi kuwa jinsia ya kiume ina nguvu na ni shupavu. Mofimu hii hii inapotumika katika jina lililotengewa jinsia ya kike, huleta dhana hasi. Kwa mfano, *Mogesi*, *Mokami na Mong'osi. Mogesi* ni mvunaji na Mokami ni *mkamaji*. *Mong'osi* ni anayetoroka hatari inapotokea badala ya kuikabili. Kwa mujibu wa uchanganuzi huu, maumbo ya majina haya hubainisha majukumu ambayo jinsia ya kike hutarajiwa kuyatekeleza na jamii kama inavyojitokeza katika {*Mo} gesi* na {*Mo}kami.* Aidha, maumbo ya majina ya jinsia ya kike hudhihirisha sifa zao. Mathalani, {*Mo}ng'osi* hutokana na kitenzi *ng'osa* (toroka) kinachotokana na woga au kushindwa. Hili hushamirisha imani kuwa jinsia ya kike ni yenye woga.

Kwa upande mwingine, mofimu {wa-} inapotumika katika jina lililotengewa jinsia ya kiume huleta dhana chanya na hasi kwa jinsia ya kike. Mfano, *{wa-}* katika *Wambura* na *{wa-}* katika *Wanchara*. *Wambura* huashiria utoshelevu huku *Wanchara* likiashiria upungufu. {Wa-} kwa hiyo huendeleza itikadi kuwa wanaume huzungukwa na neema huku wanawake wakiwa chanzo cha upungufu wa chakula na rasilmali katika jamii. Aidha, {wa-} katika majina ya jinsia ya kike huashiria umilikifu. Kwamba jinsia hii haiwezi kujitegemea pasipo na ile ya kiume. Mathalani, Wegesa [wa + igesa] na Weisana [wa + isana]. Jina *Wegesa* hutokana na jina *Igesa* (mavuno) huku *Weisana* likitokana na *Isana* (aina ya pango kunakochimbwa mchanga wa kubomea nyumba).

Mofimu *{ma-}* katika majina yaliyotengewa jinsia ya kiume huleta dhana ya ukubwa ambao huashiria nguvu, uwezo na ushujaa. Mathalani, {*Ma}gesa* (mavuno mengi), {*Ma}chera* (majia). Umbo hili basi hukuza itikadi kuwa jinsia ya kiume ni yenye nguvu, uwezo na ni shujaa. Hii hujitokeza pia pale jinsia hii hupewa majina ya wadudu kama vile *ngige (*nzige). *{ma}* huambikwa mwanzoni mwa mzizi wa jina la mdudu huyo kama vile *Magige* ili kuleta ile dhana ya ukubwa, nguvu na uwezo. Kwa upande mwingine jinsia ya kike wana majina yenye umbo linaloashiria umilikifu kama ilivyotajwa hapo juu – {*We}gesa* na {*We}isana*.

Umbo jingine ambalo limebainika ni *{nya-}*. Umbo hili hurejelea jinsia ya kike. Mfano, {*Nya}gonchera*, {*Nya}nkwi*. Pia, umbo hili huambatanishwa na mizizi ya wanyama na wadudu kama vile {*Nya}ngige* (nzige), {*Nya}nguru (kobe)* na *{Nya}irabu*. Kama ilivyotangulia kuelezwa, {nya-} hushamirisha hulka na majukumu ya jinsia ya kike. Kwa upande mwingine, {nya-} hubainisha sifa za jinsia ya kike pale wanapomithilishwa na wanyama wadogo au wadudu. Umbo hili huweza pia kujitokeza katika majina yaliyotengewa jinsia ya kiume. Kwa mfano, *{Nya}ngwe* ( wa chui) na *{Nya}ndwi* (wa simba). Kinachobainika ni kuwa umbo {nya-} linapotumika katika jina la jinsia ya kiume, huambatanishwa na mzizi wa jina la mnyama mkubwa mwenye sifa za nguvu na ujasiri kama simba na chui. Sifa hizi ndizo jinsia ya kiume katika jamii ya Wakuria hutarajiwa kuwa nazo.

**Hitimisho**

Makala haya yamejadili itikadi za ujinsia katika maumbo ya majina ya Wakuria. Maumbo haya hubainisha majina kijinsia, kuwa, huweka bayana yanayompasa mtu wa jinsia ya kiume na yule wa jinsia ya kike. Maumbo ya majina haya yamechanganuliwa kwa mwongozo wa Nadharia ya Onomastiki. Nadharia hii hujikita katika uchunguzi wa maumbo ya majina ikizingatiwa kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya lugha ya watu na shughuli zao za kitamaduni. Kwa hiyo, nadharia hii hulenga kusawiri wanajamii kwa misingi tofauti kutegemea mielekeo na matarajio ya kijamii. Makala haya basi, yamebainisha kuwa maumbo ya majina ya jinsia ya kiume huwasawiri kuwa wakubwa na wenye nguvu na uwezo katika jamii huku jinsia ya kike ikisawiriwa kuwa yenye majukumu mahususi katika jamii kama vile kuvuna na kukama. Aidha, maumbo haya hubainisha sifa za jinsia ya kike kama vile kutembeatembea pasipo na sababu maalumu, wapole na dhaifu kama wanyama wadogo na wadudu na wenye kupenda kupumzika. Kwa jumla, makala haya yameweza kubainisha jinsi majina katika jamii ya Wakuria huweza kuweka wanajamii katika makundi tofauti kijinsia na kukuza kila kundi kulingana na matarajio ya jamii nzima huku jinsia ya kike ikionekana kutwezwa na jinsia ya kiume kukwezwa.

**Marejeleo**

Agyekum, K. (2006). 'The Sociolinguitic of Akan Personal Names' *in Nordic Journal of African Studies* 15(2): 206 – 235.

Allagbe, A. A. (2016). 'Character Naming and Authorial Attitudes in Contemporary African Literature' in Research on *Humanities and Social Sciences* Vol.6, No.4

Barry, H na Herper, S. A. (2013). 'National Differences in Personality and Predictability of Gender from Personal Names' in *Cross – Cultural Research* 47(4), 363 – 371. SAGE.

Gitau, H. N. (2012). "A Semantic Analysis of Gikuyu Nouns using the Semantic Field Theory". Thesis (M.A). University of Nairobi (Haijachapishwa).

Gudeta, T. G. (2014). 'Morphosemantic Analysis of Oromo Personal Nouns' in *International Journal of Innovative Research and Development,* 3(13) pp 252-259.

Jauro, L. B. na Wenzake. (2013). 'A Morphosemantic Analysis of the Kamue Personal Names' in *International Journal of English Language and Linguistic Research* Vol.1 No.2 pg 1-12.

Kehore, Y. na Hokororo, J. (2008). *Sarufi ya Maumbo ya Kiswahili Sanifu: Sekondari na Vyuo*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. TUKI.

Kothari, C. (2008). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: New Age International Publishers.

Malande, J. (2011). 'What's in a name? An analysis of the Semantics of Lulogooli Personal Nouns' in International Journal of Humanities and Social Sciences1(20), pp 211-218.

Marjie-Okyere, S. (2015). 'A linguistic Survey of Types of Names among the Babukusu of Kenya' in *Global Journal of Human- Social Sciences*. 15(3), pp35-42

Massamba, D.P.B (2009). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha, 2nd ed.* Dar es Salaam: TUKI.

Mbiti, J. S. (1991). *Introduction to Arican Religion, 2nd ed.* Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

Mphela, K.L. (2010). "An Analysis of Personal Naming in the Moletjie Area of the Limpopo Province. An Onomastic Approach". Thesis (MA). University of Limpopo (Unpublished).

Mutegi, D. M. (2017). "Onomastiki ya Majina ya Pekee miongoni mwa Wameru Katika Tarafa ya Mwimbi Jimbo la Tharaka Nithi, Kenya". Tasnifu (Uzamili) Chuo Kikuu cha Egerton (Haijachapishwa).

Muzale, H. R. T. (1998). 'Linguistic and Socio-Cultural Aspects in Interlacustrine Bantu Names'. 61: 28-52

Okal, O. B. (2018). 'A Linguistic Overview of the Patronymic and Gender Names amongst the Selected African Communities' in *American Journal of Linguistics* 2018,6(1); 9 - 14

Riro, M. S. (2012). *Dafina ya Lugha: Isimu na Nadharia kwa Sekondari, Vyuo vya Kati na Vyuo Vikuu*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers (T) LTD.

Rossiland, F.(1990). *Marxism and Ideology*. Oxford: Clarendon Press.

Ruth, F. (1992). *Oral Literature in Africa*. Nairobi: Oxford University.

Wamitila, K. W. (1999). *"What is A Name: Towards Literary Onomastics* in Kiswahili Literature." in AAP 60.